



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



Tarehe: 6 Julai, 2023

**TANGAZO LA MNADA WA MALI CHAKAVU**

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia Wananchi wote kuwa siku ya Jumatano tarehe 19 Julai, 2023 itauza kwa njia ya mnada wa hadhara mali chakavu.


Mnada utafanyika katika ofisi za Tume zilizopo Bohari Kuu ya Serikali eneo la GPSA, Dar-es-Salaam. Mali chakavu zitakazouzwa ni pamoja na vifaa vya TEHAMA (ICT Equipment) na vifaa vya ofisi (Office Equipment).

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inawakaribisha watu wote wenye nia ya kushiriki katika mnada huo tarehe 17 na 18 Julai, 2023 katika ofisi za Tume zilizopo Dar-es-Salaam kwa ajili ya ukaguzi wa mali chakavu.

**MASHARTI YA MNADA**

1. Wananchi wataruhusiwa kukagua mali chakavu kwa siku mbili kabla ya tarehe ya mnada husika.
2. Kila mnunuzi wa mali chakavu atatakiwa kulipia mali anayotegemea kununua mara tu baada ya kutangazwa na dalali kuwa mshindi.
3. Mnunuzi atatakiwa kuondoa au kuchukua mali chakavu mara baada ya kukamilisha malipo.

4. Mali chakavu ambayo haitalipiwa kwa muda huo itanadiwa upya.
5. Malipo yatafanyika kwa asilimia 100 baada ya kuuzwa.
6. Mnunuzi atatakiwa kulipa asilimia 100 ya malipo kabla ya kuchukua mali chakavu.
7. Mnada utanza saa nne (4:00) asubuhi siku ya Jumatano tarehe 19 Julai, 2023 katika ofisi za Tume ya Taifa ya Uchaguzi zilizopo Bohari Kuu eneo la GPSA, Temeke Dar-es-Salaam.



Emmanuel Kawishe

**KAIMU MKURUGENZI WA UCHAGUZI**